

ENGLISH

SUMMARY OF THE LOCAL STAKEHOLDER CONSULTATION MEETING IN KENYA CONDUCTED BETWEEN 7th APRIL AND 10th APRIL 2026 BY BURN

INTRODUCTION

Burn Manufacturing Co, its affiliates and related entities (BURN) is inviting stakeholders to review the outcomes of the Local Stakeholder Consultations that took place from 7th April 2026 to 10th April 2026 in Nyeri, Nairobi and Kisumu Counties Kenya. During the stakeholder meetings, BURN introduced its clean cookstove Carbon Project Activities which entails “Distribution of 100,000 IoT-enabled Electric Induction Cookstoves across targeted Urban and Peri-urban areas in Kenya”.

MINUTES OF THE MEETINGS:

Registration:

Participants arrived and were asked to sign the attendance list. Participants attending through Zoom Link for the Meeting registered online to access the meeting.

Welcome Remarks:

Participants in person were welcomed by BURN team Leads for all the meetings. Introductions of the present participants were done for both the physical Meetings and the those who had joined online. The purpose of the meeting and the agenda were explained to the audience.

Project Presentation:

BURN staff started the presentation by explaining the project in detail; they presented the overview of BURN, the main goals of the program and its benefits for the local communities, as well as the ICS technology involved in the project. They also took time to remind the stakeholders about climate change and its causes, and they briefly explained the theory of the carbon credits, carbon markets and the development of carbon projects. BURN team took some time to explain carefully to the stakeholders that the transfer of rights to the carbon credits generated using the stoves would be transferred to BURN as the Project Proponent of the entire project. The carbon waiver was demonstrated to be a formal agreement signed by the end user

upon purchasing the stove. By the end user signing this Carbon Waiver Agreement they would be waiving their claims to any Internationally Transferred Mitigation Outcomes (ITMOs) generated using that stove. The purpose for this and the way in which BURN would use the revenues from the sale of the carbon credits was explained clearly in the presentation during the LSC meeting.

Questions and answers session:

Stakeholders raised many questions about the price of the ICS and its quality, as well as the expected timeline for the project and the distribution plans. They expressed a lot of interest in the involvement of the communities and more particularly the involvement of women. All these questions and comments were fully and satisfactorily answered by the project proponents.

Presentation of the Safeguarding Principles and Sustainability assessment of the project:

BURN staff explained the project's Safeguarding Principles and their assessment. The stakeholders were continuously consulted for feedback and comments, as an open discussion. The meeting continued with a presentation of the SDGs, and on the positive impacts of the project on a few specific SDGs. Participants agreed with the assessment and did not have further comments. BURN staff presented the grievance mechanism as well as how the sustainable development impacts will be monitored.

Closure of the meeting:

The evaluation forms were then distributed to the participants. The team expressed its appreciation to all participants who attended the meeting and who offered many constructive suggestions. The meeting closed with a demonstration of the BURN Induction Cooker.

COMMENTS RECEIVED DURING THE STAKEHOLDER MEETING

Gender of Stakeholder	Stakeholder comment	Was comment taken into account (Yes/No)?	Explanation (Why? How?)
F	Can the top glass of the IDC break?	Yes	The IDC glass top is made from highly reinforced tempered glass which does not easily break even under high heat. The glass can however break if mishandled e.g. using it as a surface to place heavy items that are not pots
M	How many kilowatts does the IDC use per day	YES	The IDC has a maximum capacity of 2,000w. Consumption depends on the usage of the IDC. Customers are advised to mostly use medium and low power settings for efficient consumption.
M	If I bought the stove and relocated to a different region, will I get assistance from my new location?	Yes	Yes, you can use the stove anywhere, not necessarily the location where you bought it. You will also get assistance from your new location. This is because the project is being implemented within the entire country in the urban and peri-urban regions.
M	What happens when power goes off and I was cooking on the IDC, does it continue cooking or does it go off?	Yes	The IDC uses electricity to power it. If electricity goes off, the IDC also shuts down. Its smart technology enables the IDC to also detect high voltage and low voltage to ensure

Gender of Stakeholder	Stakeholder comment	Was comment taken into account (Yes/No)?	Explanation (Why? How?)
			electric faults do not cause a safety risk to users
M	Are there health effects to users due to the electromagnetic waves?	Yes	No, the IDC has no negative health impacts to users. The electromagnetic waves conduct heat between the stove and the pot and are only active when cooking is happening.
M	Does the Induction Cooker stove use Solar?	Yes	BURN induction Cooker stove purely uses Electricity.
F	If I pay for 2 months then miss payment, will the cost increase?	Yes	No, the initial cost of the IDC does not increase in the case of missed payment, it only affects the repayment period which increases.
F	For the safety feature on child lock, is it sensitive to only the person who locked it or can anyone unlock it?	Yes	The child lock safety feature is not sensitive to only the person who purchased the cooker but can also be used by other members of the household. The feature enhances safety by ensuring the cooking settings are not tampered with by children.
F	Incase someone wants to purchase the induction cooker in cash, can that	Yes	Carbon subsidies enable BURN to provide the IDC at affordable prices for both the pay as you cook plan and cash prices. As such, the current

Gender of Stakeholder	Stakeholder comment	Was comment taken into account (Yes/No)?	Explanation (Why? How?)
person get some discounts?			prices being offered are already subsidized.
M	For durability, how long does the IDC last?	Yes	The IDC has a 7–10-year lifespan and can last longer based on how the household uses their stove. Households who procure these cookstoves are provided with a 1-year warranty and access to repair stoves through BURN’s customer experience team and local service hubs throughout the life of the stove.
F	Can I cook Githeri on the IDC?	Yes	Yes, you can cook all types of foods on the IDC without restriction. It also comes with an anti-slippery silicone mat that ensures the pot remains stable when preparing foods like ugali
F	Are there stoves that have more than one plate where I can cook more than 1 pot at a time?	Yes	Currently, the IDC has only one plate, however the research development team are exploring options for further future expansion
M	What are the drawbacks of this Project?	Yes	The IDC uses electricity to power it, users who are not connected to a stable electric grid are not able to use the IDC.

Gender of Stakeholder	Stakeholder comment	Was comment taken into account (Yes/No)?	Explanation (Why? How?)
F	What is the durability of the sensor and what kind of information does it record? Is it prone to thermal heat damage?	Yes	The sensor records usage data. It can detect every time there is a cooking activity and records the time spent cooking and the power consumption. The sensor is not prone to thermal heat damage.
F	Can I get access to more sufurias for the IDC	Yes	Yes, you can purchase extra pots for the IDC from BURN or from other vendors that sell ferromagnetic pots.
F	If I need this Induction cooker, how can I get it?	Yes	Stove distribution for the project is set to begin in June 2026. Distribution will be done through sales and field agents who do home deliveries and train the user on the cooker. You can also reach BURN on the contact number provided.

SUMMARY OF THE ASSESSMENT OF SAFEGUARDING PRINCIPLES

It was explained during the meeting that the aim of the project is to disseminate highly efficient clean cookstoves that would reduce the amount of charcoal and firewood used by households. By this, the project would have positive social, economic, and environmental impacts. The project will follow all safeguarding principles as described in the table below

Safeguarding Principle	Assessment
------------------------	------------




<p>Human Rights</p>	<p>The Project respects internationally proclaimed human rights and is not complicit in violence or human rights abuses of any kind as defined in the Universal Declaration of Human Rights. The project will not discriminate with regards to participation and inclusion.</p>
<p>Gender Equality and Women’s Rights</p>	<p>The Mitigation Activity does not endorse any form of discrimination based on gender. The project will take into account gender roles and the abilities of women and men to participate in the decision/design of all aspects of the programme.</p>
<p>Community Health, Safety and Working Conditions</p>	<p>The project will not expose the community to increased health risks and is not adversely affecting the health of the workers and the community.</p>
<p>Cultural Heritage, Indigenous Peoples, Displacement and Resettlement</p>	<p>The project activity will not have any negative impact on cultural heritage, indigenous people nor will it displace or resettle people.</p>
<p>Corruption</p>	<p>The Project doesn’t involve, be complicit in or inadvertently contribute to or reinforce corruption or corrupt Projects.</p>
<p>Economic Impacts</p>	<p>The project will respect all labour rights. No negative economic consequences are expected from the project activity. On the contrary, it is expected that the project contributes to sustainable economic growth.</p>



Climate and Energy	The project will reduce GHG emissions as will be monitored and verified in line with the carbon standard requirements
Water	The project will not affect natural water patterns/flows or cause any additional erosion and/or water body instability.
Environment, ecology and land use	The project will not have any negative impact on the environment and ecology and will not involve the use of land and soil for production of crops or other products. The release of particulate matters and carbon monoxide are significantly reduced by the introduction of improved (more efficient) cookstoves.




The assessment process was interactive and participative. The stakeholders fully agreed with the assessment done by BURN.

SUMMARY OF SUSTAINABILITY ASSESSMENT

This Project is to contribute to different Sustainable Development Goals (SDGs) in the following way:

SDGs	Targets	Proposed monitoring Indicator
 <p>1 NO POVERTY</p>	<p>1.4 By 2030, ensure that all men and women, the poor and the vulnerable, have equal rights to economic resources, as well as access to basic services, ownership and control over land and other forms of property, inheritance, natural resources, appropriate new technology and financial services, including microfinance.</p>	<p>Monetary savings related to the purchase of cooking fuels</p> <p>Surveys will be carried out to check on the money spent for purchasing cooking fuels in the project scenario compared to the baseline scenario.</p>
 <p>3 GOOD HEALTH AND WELL-BEING</p>	<p>3.9 By 2030, substantially reduce the number of deaths and illnesses from hazardous chemicals and air, water and soil pollution and contamination.</p>	<p>Perceived air quality</p> <p>Surveys will be carried out to check on the pollution-related inconveniences (such as smoke levels, itchy eyes and breathing problems) in the project scenario compared to the baseline scenario.</p>
 <p>4 QUALITY EDUCATION</p>	<p>4.3 By 2030, substantially increase opportunities to ensure inclusive and equitable quality education and promote lifelong learning opportunities for all</p>	<p>Number of people receiving skill development training</p>

SDGs	Targets	Proposed monitoring Indicator
 <p>5 GENDER EQUALITY</p>	<p>5.4 By 2030, Achieve gender equality and empower all women and girls</p>	<p>The ICS shortens cooking time and frees up time spent on unpaid labour. It also reduces the frequency of fuel purchases. This then creates time savings, particularly for women and girls, who provide unrecognized labor associated with fuel collection and meal preparation, creating time that can be used for other activities.</p>
 <p>7 AFFORDABLE AND CLEAN ENERGY</p>	<p>7.1 By 2030, ensure universal access to affordable, reliable, and modern energy for all.</p> <p>7.B By 2030, expand infrastructure and upgrade technology for supplying modern and sustainable energy services for all in developing countries, least developed countries, small island developing States, and land-locked developing countries, in accordance with their respective programmes of support</p>	<p>Number of sold/distributed ICS in use</p> <p>The total number of ICS sold/distributed is summed up in the database, discounting the number of households who stop using the ICS</p>

SDGs	Targets	Proposed monitoring Indicator
	<p>8.5 By 2030, achieve full and productive employment and decent work for all women and men, including for young people and persons with disabilities, and equal pay for work of equal value.</p>	<p>Number of jobs created</p>
	<p>13.3 Improve education, awareness-raising and human and institutional capacity on climate change mitigation, adaptation, impact reduction and early warning.</p>	<p>CO2 emission reductions achieved by the project activity</p>
	<p>15.3 By 2030, Protect, restore, and promote sustainable use of terrestrial ecosystems, sustainably manage forests, combat desertification, and halt and reverse land degradation and halt biodiversity loss</p>	<p>Reduction in firewood and charcoal. Surveys and monitoring of firewood consumption trends in project households compared to baseline households to assess impact on forest resources.</p>

Stakeholders' sustainable development assessment was fully in line with BURN'S own assessment. In terms of the monitoring of the sustainable development indicators, the stakeholders did not have other comments or suggestions related to the monitoring of the sustainable development indicators. They agreed to proceed with the indicators selected by BURN.

CONTACT US:

If you wish to get in touch with the project for more information, please contact us at:

	Method Chosen (include all known details e.g. location of book, phone, number, identity of mediator)	Justification of Choice (best practice)
Continuous Input / Grievance Expression Process Book (mandatory)	1. BURN Manufacturing, Ruiru Office - Ruiru Business Park (RBP) factory office, Lat 1.145716, long 36.950604	The stakeholders were pleased to have an input book opened at the office in Ruiru. Complaints or any other concerns can be stated and will be filed directly at the head office.
Telephone access (optional)	Toll Free Number; (+254) 700 667 788 SMS: 22876 WhatsApp: +254768473017	The phone number of BURN Kenyan offices were made known to all project beneficiaries
Internet/email access (optional)	info@burnmfg.com	BURN email address will be made known to all project beneficiaries

SWAHILI VERSION

MUHTASARI WA MKUTANO WA USHAURI NA WADAU WA NDANI NCHINI KENYA ULIOFANYIKA KATI YA TAREHE 7 APRILI HADI 10 APRILI 2026 NA BURN UTANGULIZI

Burn Manufacturing Co, washirika wake na taasisi zinazohusiana (BURN) inawaalika wadau kupitia na kutoa maoni kuhusu matokeo ya Ushauri na Wadau wa Ndani uliofanyika kuanzia tarehe 7 Aprili 2026 hadi 10 Aprili 2026 katika kaunti za Nyeri, Nairobi na Kisumu nchini Kenya. Wakati wa mikutano hiyo, BURN ilitambulisha shughuli zake za Mradi wa Kaboni wa majiko safi ya kupikia, unaohusisha “Usambazaji wa majiko 100,000 ya umeme ya induction yaliyounganishwa na teknolojia ya IoT katika maeneo yaliyolengwa ya mijini na pembezoni mwa miji nchini Kenya.”

MUHTASARI WA YALIYOJADILIWA KWENYE MIKUTANO:

Usajili:

Washiriki walifika na kuombwa kusaini orodha ya mahudhurio. Washiriki waliohudhuria kupitia kiungo cha Zoom walijisajili mtandaoni ili kuweza kushiriki kwenye mkutano.

Maneno ya Karibu:

Washiriki waliohudhuria ana kwa ana walikaribishwa na viongozi wa timu ya BURN katika mikutano yote. Utambulisho wa washiriki ulifanyika kwa wale waliokuwepo ukumbini pamoja na wale waliojiunga mtandaoni. Madhumuni ya mkutano na ajenda yalielezwa kwa washiriki.

Uwasilishaji wa Mradi:

Wafanyakazi wa BURN walianza uwasilishaji kwa kuelezea mradi kwa kina; waliwasilisha muhtasari wa BURN, malengo makuu ya programu na faida zake kwa jamii za wenyeji, pamoja na teknolojia ya majiko safi (ICS) inayotumika katika mradi. Pia walichukua muda kuwakumbusha wadau kuhusu mabadiliko ya tabianchi na sababu zake, na walielezea kwa ufupi dhana ya mikopo ya kaboni, masoko ya kaboni na maendeleo ya miradi ya kaboni.

Timu ya BURN pia ilichukua muda kuelezea kwa kina kwa wadau kwamba haki za mikopo ya kaboni inayozalishwa kupitia matumizi ya majiko hayo zitahamishiwa kwa BURN kama mhusika mkuu wa mradi mzima. Fomu ya kuachia haki za kaboni ilionyeshwa kama makubaliano rasmi yanayosainiwa na mtumiaji wa mwisho wakati wa kununua jiko. Kwa

kusaini makubaliano haya, mtumiaji anakubali kuachia haki zake zozote za madai ya upunguzaji wa uzalishaji wa hewa chafu uliothibitishwa unaotokana na matumizi ya jiko hilo.

Madhumuni ya hatua hii na namna BURN itakavyotumia mapato yatoakanayo na uuzaji wa mikopo ya kaboni yalielezwa kwa uwazi wakati wa uwasilishaji katika mkutano wa Ushauri na Wadau wa Ndani (LSC).

Kipindi cha Maswali na Majibu:

Wadau waliuliza maswali mengi kuhusu bei ya majiko ya ICS na ubora wake, pamoja na muda unaotarajiwa wa utekelezaji wa mradi na mipango ya usambazaji. Walionyesha pia hamasa kubwa kuhusu ushirikishwaji wa jamii, hasa zaidi ushirikishwaji wa wanawake.

Maswali na maoni haya yote yalijibiwa kikamilifu na kwa kuridhisha na waandaaji wa mradi.

Uwasilishaji wa Kanuni za Ulinzi na Tathmini ya Uendeleu ya Mradi:

Wafanyakazi wa BURN walielezea Kanuni za Ulinzi za mradi pamoja na tathmini yake. Wadau waliendelea kushirikishwa kikamilifu kwa kutoa maoni na mrejesho kupitia mjadala wa wazi.

Mkutano uliendelea kwa uwasilishaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), pamoja na athari chanya za mradi kwa baadhi ya malengo hayo. Washiriki walikubaliana na tathmini hiyo na hawakuwa na maoni ya ziada.

Wafanyakazi wa BURN pia waliwasilisha utaratibu wa kushughulikia malalamiko pamoja na namna athari za maendeleo endelevu zitakavyofuatiliwa.

Kufungwa kwa Mkutano:

Fomu za tathmini zilisambazwa kwa washiriki. Timu ilitoa shukrani zake kwa washiriki wote waliohudhuria mkutano na kutoa mapendekezo yenye kujenga. Mkutano ulifungwa kwa onyesho la Induction Cooker.

MAONI YALIYOPOKELEWA WAKATI WA MKUTANO WA WADAU

Jinsia ya Mdau	Maoni ya Mdau	Je, Maoni Yalizingatiwa (Ndiyo/Hapana) ?	Maelezo (Kwa nini? Vipi?)
F	Je, kioo cha juu cha jiko la IDC kinaweza kuvunjika?	Ndiyo	Sehemu ya juu ya kioo cha IDC imetengenezwa kwa kioo kigumu cha <i>tempered</i> chenye uimara wa hali ya juu ambacho hakivunjiki kirahisi hata chini ya joto kali. Hata hivyo, kinaweza kuvunjika kikitumika vibaya, kwa mfano kutumika kama sehemu ya kuweka vitu vizito ambavyo si vyombo vya kupikia.
M	Jiko la IDC linatumia kilowati ngapi kwa siku?	Ndiyo	IDC lina uwezo wa juu wa wati 2,000. Matumizi halisi hutegemea namna jiko linavyotumika. Wateja wanashauriwa kutumia viwango vya kati na vya chini vya umeme ili kupunguza matumizi.
M	Nikinunua jiko kisha nikahamia eneo lingine, nitapata msaada huko?	Ndiyo	Ndiyo, unaweza kutumia jiko popote, si lazima pale ulipolinunua. Pia utapata msaada katika eneo jipya kwani mradi unatekelezwa nchi nzima katika maeneo ya mijini na pembezoni mwa miji.
M	Kuna athari za kiafya kutokana na mawimbi ya sumakuumeme?	Ndiyo	Hapana, IDC haina athari mbaya kiafya kwa watumiaji. Mawimbi ya sumakuumeme hutumika kuhamisha joto kati ya jiko na chombo cha

Jinsia ya Mdau	Maoni ya Mdau	Je, Maoni Yalizingatiwa (Ndiyo/Hapana) ?	Maelezo (Kwa nini? Vipi?)
			kupikia na hufanya kazi tu wakati wa kupika.
M	Je, jiko la induction linatumia nishati ya jua (solar)?	Ndiyo	Jiko la induction la BURN linatumia umeme pekee.
F	Nikilipia kwa miezi miwili kisha nikakosa kulipa, gharama itaongezeka?	Ndiyo	Hapana, gharama ya awali ya IDC haiongezeki ukikosa malipo. Kinachoathirika ni muda wa marejesho ambao huongezeka.
F	Kuhusu kipengele cha usalama cha <i>child lock</i> , kinafunguliwa na aliyekifunga tu au mtu yeyote anaweza kufungua?	Ndiyo	Kipengele hiki hakimtegemei mtu mmoja tu; wanafamilia wengine wanaweza kukitumia. Kinaongeza usalama kwa kuzuia watoto kubadilisha mipangilio ya kupikia.
F	Kama mtu anataka kununua kwa pesa taslimu, anaweza kupata punguzo?	Ndiyo	Ruzuku ya kaboni inaiwezesha BURN kutoa IDC kwa bei nafuu kwa mpango wa <i>lipa unapotumia</i> na pia kwa bei ya taslimu. Hivyo, bei zilizopo tayari zimepunguzwa.
M	Kwa uimara, IDC hudumu kwa muda gani?	Ndiyo	IDC ina muda wa matumizi wa miaka 7-10. Watumiaji hupata dhamana ya mwaka 1 na huduma za matengenezo kupitia timu ya huduma kwa wateja ya BURN na vituo vya huduma vya karibu.

Jinsia ya Mdau	Maoni ya Mdau	Je, Maoni Yalizingatiwa (Ndiyo/Hapana) ?	Maelezo (Kwa nini? Vipi?)
M	Changamoto za mradi huu ni zipi?	Ndiyo	IDC hutumia umeme, hivyo watumiaji wasiokuwa na umeme wa uhakika hawawezi kulitumia.
F	Uimara wa kihisi (sensor) ukoje na kinarekodi taarifa gani? Je, kinaweza kuathiriwa na joto kali?	Ndiyo	Kihisi hurekodi taarifa za matumizi, ikiwa ni pamoja na kila tukio la kupika, muda uliotumika na kiasi cha umeme kilichotumika. Hakiharibiki kirahisi kutokana na joto.
F	Naweza kupata sufuria zaidi zinazotumika na IDC?	Ndiyo	Ndiyo, unaweza kununua sufuria za ziada kutoka BURN au kwa wauzaji wengine wanaouza vyombo vinavyovutwa na sumaku (<i>ferromagnetic</i>).
F	Nikitaka kununua jiko la induction, nitapataje?	Ndiyo	Usambazaji wa majiko unatarajiwa kuanza Juni 2026. Utatekelezwa kupitia mawakala wa mauzo na maafisa wa uwanjani watakaofanya usambazaji wa majumbani pamoja na kutoa mafunzo ya matumizi kwa mtumiaji.

MUHTASARI WA TATHMINI YA KANUNI ZA ULINZI

Ilielezwa wakati wa mkutano kwamba lengo la mradi ni kusambaza majiko safi ya kupikia yenye ufanisi wa juu ambayo yatapunguza matumizi ya mkaa na kuni katika kaya. Kupitia

hili, mradi utakuwa na athari chanya za kijamii, kiuchumi na kimazingira. Mradi utafuata kanuni zote za ulinzi kama zilivyoielezwa kwenye jedwali hapa chini.



Kanuni ya Ulinzi	Tathmini
Haki za Binadamu	Mradi unaheshimu haki za binadamu zinazotambuliwa kimataifa na hauhusiki kwa njia yoyote na vitendo vya ukatili au ukiukwaji wa haki za binadamu kama ilivyoainishwa katika Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu. Mradi hautabagua katika masuala ya ushiriki na ujumuishaji.
Usawa wa Kijinsia na Haki za Wanawake	Shughuli za mradi hazihusishi wala kuunga mkono aina yoyote ya ubaguzi wa kijinsia. Mradi utazingatia majukumu ya kijinsia na uwezo wa wanawake na wanaume kushiriki katika maamuzi na usanifu wa shughuli za mradi. Itahakikisha kuwa wanawake (ikiwemo vikundi vya wanawake) na wanaume wanaalikwa kushiriki katika mashauriano ya wadau ili kuwa na uwakilishi wa kutosha wa jinsia zote katika mikutano ya ushauri wa wadau wa ndani..
Afya, Usalama wa Jamii na Hali za Kazi	Mradi hautawaweka wanajamii katika hatari kubwa za kiafya na hautaathiri vibaya afya ya wafanyakazi pamoja na jamii kwa ujumla.
Urithi wa Kitamaduni, Watu wa Asili, Uhamishaji na Makazi Mapya	Shughuli za mradi hazitakuwa na athari zozote hasi kwa urithi wa kitamaduni wala watu wa asili, na pia hazitasababisha uhamishaji au kuwahamisha watu kutoka makazi yao.



Rushwa	Mradi hauhusiki, hautashiriki, wala hautachangia kwa njia yoyote katika vitendo vya rushwa au miradi yenye rushwa.
Athari za Kiuchumi	Mradi utaheshimu haki zote za wafanyakazi. Hakuna athari hasi za kiuchumi zinazotarajiwa kutokana na shughuli za mradi. Kinyume chake, unatarajiwa kuchangia ukuaji wa uchumi endelevu.
Hali ya Hewa na Nishati	Mradi utapunguza uzalishaji wa gesi chafu (GHG) kama itakavyofuatiliwa na kuthibitishwa kulingana na mahitaji ya viwango vya kaboni.
Maji	Mradi hautaathiri mifumo ya asili ya mtiririko wa maji wala kusababisha mmomonyoko wa ardhi au kuyumbisha vyanzo vya maji.
Mazingira, Ikolojia na Matumizi ya Ardhi	Mradi hautakuwa na athari hasi kwa mazingira na ikolojia, na hautahusisha matumizi ya ardhi au udongo kwa ajili ya uzalishaji wa mazao au bidhaa nyingine. Uzalishaji wa chembechembe hewani (particulate matter) na gesi ya monoksidi ya kaboni utapungua kwa kiasi kikubwa kupitia matumizi ya majiko bora zaidi yenye ufanisi wa juu.




Mchakato wa tathmini ulikuwa shirikishi na jumuishi. Wadau walikubaliana kikamilifu na tathmini iliyofanywa na BURN.

MUHTASARI WA TATHMINI YA UENDELEVU

Mradi huu unalenga kuchangia Malengo mbalimbali ya Maendeleo Endelevu (SDGs) kwa namna zifuatazo:

SDGs	Malengo ya SDGs	Kiashiria Kilichopendekezwa cha Ufuatiliaji
	<p>1.4 Kufikia mwaka 2030, kuhakikisha kwamba wanaume na wanawake wote, hususan maskini na walio katika mazingira hatarishi, wanakuwa na haki sawa za rasilimali za kiuchumi, pamoja na upatikanaji wa huduma za msingi, umiliki na udhibiti wa ardhi na mali nyingine, urithi, rasilimali za asili, teknolojia mpya zinazofaa na huduma za kifedha ikiwemo mikopo midogo (microfinance).</p>	<p>Akiba ya kifedha inayotokana na ununuzi wa nishati ya kupikia Utafiti utafanywa ili kufuatilia kiasi cha fedha kinachotumika kununua nishati ya kupikia katika hali ya mradi ikilinganishwa na hali ya awali (baseline).</p>
	<p>3.9 Kufikia mwaka 2030, kupunguza kwa kiasi kikubwa vifo na magonjwa yatokanayo na kemikali hatarishi pamoja na uchafuzi wa hewa, maji na udongo.</p>	<p>Ubora wa hewa unaotambulika Tafiti zitafanywa ili kuchunguza athari za uchafuzi (kama vile kiwango cha moshi, kuwasha macho na matatizo ya kupumua) katika hali ya mradi ikilinganishwa na hali ya awali.</p>

SDGs	Malengo ya SDGs	Kiashiria Kilichopendekezwa cha Ufuatiliaji
	<p>4.3 Kufikia mwaka 2030, kuongeza kwa kiasi kikubwa fursa za kuhakikisha elimu bora, jumuishi na yenye usawa, na kuhamasisha fursa za kujifunza maisha yote kwa wote.</p>	<p>Idadi ya watu wanaopata mafunzo ya kukuza ujuzi</p>
	<p>5.4 Kufikia mwaka 2030, kufikia usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake na wasichana wote.</p>	<p>Ufanisi wa muundo wa majiko bora ya kupikia hupunguza muda wa kuandaa chakula na kupunguza mara za kununua mafuta ya kupikia. Hali hii huokoa muda, hasa kwa wanawake na wasichana ambao mara nyingi hubeba mzigo wa kazi usiotambuliwa unaohusiana na ukusanyaji wa kuni na maandalizi ya chakula. Muda huu unaokolewa unaweza kutumika katika shughuli zenye tija kama vile mafunzo, shughuli za kijamii au ushiriki katika maendeleo ya jamii.</p>

SDGs	Malengo ya SDGs	Kiashiria Kilichopendekezwa cha Ufuatiliaji
	<p>7.1 Kufikia mwaka 2030, kuhakikisha upatikanaji wa huduma za nishati nafuu, za kuaminika na za kisasa kwa wote.</p> <p>7.B Kufikia mwaka 2030, kupanua miundombinu na kuboresha teknolojia kwa ajili ya kusambaza huduma za nishati ya kisasa na endelevu kwa wote katika nchi zinazoendelea, zikiwemo nchi zilizoendelea kidogo, nchi za visiwa vidogo zinazoendelea na nchi zisizo na bandari, kwa kuzingatia programu zao za msaada.</p>	<p>Idadi ya majiko ya ICS yaliyouzwa/kusambazwa na yanayotumika</p> <p>Jumla ya majiko ya ICS yaliyosambazwa itahesabiwa kupitia hifadhidata ya mradi.</p>
	<p>8.5 Kufikia mwaka 2030, kufikia ajira kamili na yenye tija pamoja na kazi zenye staha kwa wanawake na wanaume wote, wakiwemo vijana na watu wenye ulemavu, na malipo sawa kwa kazi yenye thamani sawa.</p>	<p>Idadi ya ajira zitakazoundwa.</p>
	<p>13.3 Kuboresha elimu, uhamasishaji na uwezo wa watu na taasisi katika kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, kuhimili athari zake, kupunguza madhara na mifumo ya tahadhari ya mapema.</p>	<p>Upunguzaji wa uzalishaji wa hewa ya CO₂ unaofikiwa na shughuli za mradi</p>

SDGs	Malengo ya SDGs	Kiashiria Kilichopendekezwa cha Ufuatiliaji
	<p>15.3 Kufikia mwaka 2030, kulinda, kurejesha na kuhamasisha matumizi endelevu ya mifumo ya ikolojia ya ardhini, kusimamia misitu kwa njia endelevu, kupambana na kuenea kwa jangwa, kusitisha na kurejesha uharibifu wa ardhi, na kusitisha upotevu wa bioanuwai.</p>	<p>Upunguzaji wa matumizi ya kuni na mkaa Utafiti na ufuatiliaji wa mwenendo wa matumizi ya kuni katika kaya za mradi ukilinganishwa na kaya za msingi (baseline) utafanywa ili kutathmini athari kwa rasilimali za misitu</p>

Tathmini ya wadau kuhusu maendeleo endelevu ililingana kikamilifu na tathmini ya BURN. Kuhusu ufuatiliaji wa viashiria vya maendeleo endelevu, wadau hawakuwa na maoni au mapendekezo ya ziada. Walikubaliana kuendelea kutumia viashiria vilivyochaguliwa na BURN.

WASILIANA NASI:

Iwapo ungependa kuwasiliana na mradi kwa maelezo zaidi, tafadhali tumia njia zifuatazo:

	Njia Iliyochaguliwa (jumuisha maelezo yote muhimu kama eneo la kitabu, nambari ya simu, utambulisho wa mpatanishi	Sababu ya Uchaguzi (mbinu bora)
Kitabu cha Maoni Endelevu (Continuous Input / Grievance Book)	BURN Manufacturing, Ofisi ya Ruiru – Kiwanda cha Ruiru Business Park (RBP), Lat 1.145716, Long	Wadau walifurahishwa na uwepo wa kitabu cha maoni katika ofisi ya Ruiru. Malalamiko au hoja zozote zinaweza

	36.950604	kuwasilishwa na zitashughulikiwa moja kwa moja katika ofisi kuu.
Mawasiliano ya Simu	Nambari ya Bure: (+254) 700 667 788 SMS: 22876 WhatsApp: +254 768 473 017	Nambari za simu za ofisi za BURN nchini Kenya zilitolewa kwa wanufaika wote wa mradi.
Mtandao/Barua Pepe (Hiari)	info@burnmfg.com	Anwani ya barua pepe ya BURN itatolewa kwa wanufaika wote wa mradi